**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**CHUO CHA UALIMU MONDULI**

SLP 5, MONDULI.
Simu: +255 (0)27 2538026
Fax +255 (0)27 2538060
Web: www.mondulitc.ac.tz
Email:<mondulitc@gmail.com>

---

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO NGAZI YA STASHAHADA MAALUMU YA UALIMU ELIMU MSINGI MIAKA MITATU - 2025/2026.**

1. **UTANGULIZI**

Chuo cha Ualimu Monduli ni moja ya vyuo kongwe katika utoaji wa mafunzo ya ualimu katika ngazi ya Stashahada.

**Dira ya Chuo** ni "Chuo cha Ualimu Monduli kinatazamiwa kuwa Chuo bora chenve kutumia sayansi na teknolojia katika kutoa elimu yenye kuhimiza uweledi na ujuzi wa utendaji kazi kwa wahitimu".

**Kauli yetu** ni "Elimu ni Ukombozi". Elimu bora ni ile inayomsaidia mtu, kujiendeleza na kujikomboa kutokana na vipingamizi vilivyomo katika mazingira yake. Tunategemea kuwa wewe utatumia nafasi hii ya mafunzo kujiendeleza kwa manufaa yako na taifa letu.

Chuo kipo mashariki ya mji wa Monduli. Mji wa Monduli upo kilometa 40 magharibi ya mji wa Arusha. Usafiri wa mabasi kutoka Arusha unapatikana kwa urahisi kuanzia saa 12.00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

2. **MAHITA.JI KWAA JILI YA USAJILI**

A. VVETI NA VITAMBULISHO

Ni lazima uoneshe hati zifuatazo ili upate usajili:

i. Cheti halisi cha Kidato cha Nne, kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania au result slip halisi kwa waliomaliza kidato cha nne mwaka 2024.
ii. School Leaving Certificate ya Kidato cha Nne.
iii. Cheti cha kuzaliwa.
vi. Picha nne (4) za passport size ziwe zimepigwa karibuni (blue background).

**Angalizo: Usajili utazingatia masomo uliyosomea na kufaulu pekee.**

## CHUO CHA UALIMU MONDULI

### B. ADA NA MICHANGO KWA WANACHUO MWAKA 2025/2026

1) **Ada:** Tsh. **450,000/=** kwa mwaka. Unaweza kulipa Tsh.**225, 000/=** kwa awamu mbili.

2) **MICHANGO**

i. Usajili na Kitambulisho Tsh. 20,000/= **kwa mwaka wa kwanza tu.**
ii. Mchango wa Serikali ya wanachuo Tsh. 5,000/ = **kwa mwaka.**
iii. Godoro: Chuo kitakuazima godoro kwa gharama ya Tshs **10,000/= kwa mwaka**.
iv. Huduma ya Kwanza Tshs 10,000 / **kwa mwaka**
**v.** Ulinzi elfu 30,000/= **kwa mwaka**
vi. Michezo Tshs 30,000/=**kwa mwaka**
vii. Usafi wa mazingira Tsh 20,000/= **kwa mwaka**
viii. Ukarabati Tsh 25,000/=**kwa mwaka**
ix. Bima ya Afya Tshs 50,400/=kwa asiye nayo **kwa mwaka**

**JUMLA TSH 200,400/=**

**Angalizo**

**(a) Ada italipwa ukifika chuoni baada ya kupewa Control Number na Mhasibu wa Chuo**


**(b) Michango ilipwe kwa mkupuo mmoja (mwanachuo anaporipoti chuoni) katika akaunti yenye jina Monduli T.C. Education Development Fund, namba 41301100001 Bank ya NMB.**

**(c)Njoo na karatasi halisi ya malipo ya michango ya Bank (Original Bank Pay Slip)**


## C. SARE

Wanachuo wote lazima wavae sare rasmi ya Chuo wakati wa masomo, shughuli rasmi na wakati wa matembezi nje ya Chuo. Sare ya Chuo hiki ni kama ifuatavyo:

- **Suruali/Sketi (2)** rangi **"dark blue plain material"**
  - **Suruali**: mshono wa kawaida, makunjo/marinda mawili mbele, mifuko isiwe ya kubandika. **Mshono: (Rejea Picha 2)**
  - **Sketi:** urefu uwe sentimeta kumi chini ya goti, isiyobana mwili/ sketi ndefu hadi chini kwa waislamu tu watakaopenda. Mshono: **(Rejea Picha 1)**
  - **Shati au blauzi (2)** rangi nyeupe mikono mirefu isiyo na nembo yoyote.
- **Sweta rangi "dark blue" V-neck** au koti (suti) lililoshonwa kwa kitambaa sawa na suruali/sketi.
  - **Tai:** Tai ndefu ya rangi nyeusi au "dark blue" (kwa wanachuo wote).
- Viatu (jozi mbili au zaidi): Viatu vya ngozi,rangi nyeusi na viwe na kamba , visiwe na visigino virefu. Makobazi hayaruhusiwi kama sare.
- **Soksi (jozi tatu au zaidi):** Rangi ya **bluu au nyeusi** kwa wanaume: rangi nyeupe kwa wanawake.
- **Mkanda:** Rangi nyeusi,uwe wa ngozi usio na madoido (Wanaume).
- **T-shirt** yenye nembo ya Chuo itapatikana chuoni (Tsh. 15, 000) Kila mwanachuo anapaswa kuwa nayo.
- **Ushungi** mweupe kwa wanawake wa kiislam (Kwa atakayependa)




**PICHA 1 MAVAZI YA KIKEA**



**PICHA NO 2: MAVAZI YA KIUME**

**Muhimu:**

- **Mavazi ya kuvaa baada ya vipindi vya darasani yawe ya heshima.**
- **Mwanachuo anapaswa kuja na sare hizo (na Sio kuja kuzishona chuoni)**

**D. MAVAZI YA MICHEZO NA BURUDANI**

Michezo ni burudani na inaimarisha afya. Kila mwanachuo lazima kushiriki katika michezo.

**Ifuatayo ni orodha ya mavazi unayopaswa kuja nayo,**

- Track suit ya rangi ya **"DARK BLUE"** kwa wanaume**," BLUE BAHARI"** kwa wanawake.
- "Jersey" nyekundu (fulana na bukta yake) na viatu vya michezo (soccer boots na raba) kwa jinsi zote.

3. **MAHITAJI MUHIMU VA TAALUMA**

i. Daftari kubwa kaunta book quire 3 (10), kalamu, penseli, rula (01) na faili (10).
ii. "Mathematical instruments"
iii. Kamusi ya Kiingereza sayansi (Dictionary).
iv. Scientific calculator kwa wanachuo wote.
v. Koti jeupe la Maabara kwa wanachuo wote.
vi. Karatasi (ream moja **A4-plain) (01)**

**Angalizo: Simu ya aina yoyote, Tablet haviruhusiwi chuoni**

**MAAGIZO MUHIMU YA AFYA**

Njoo katika mafunzo ukiwa imara kiafÿa. Fomu ya kutathimini afya iliyoambatanishwa, ijazwe kikamilifu na Daktari wa Hospitali ya Serikali.

**Kila mwanachuo LAZIMA awe na kadi ya Bima ya Afva Au aje na kiasi cha Tsh. 50,400/=**

4. **MALI BINAFSI**

**Matandiko**

i. Lete Blanketi
ii. Mto, chandarua (mviringo).
iii. Shuka mbili na foronya (2) za rangi ya pinki kwa wasichana na rangi ya blue bahari kwa wavulana
iv. Pazia la rangi ya pink lisilo na maua kwa wasichana na rangi ya blue bahari isiyo na maua kwa wavulana.

6, **MAHITAJI BINAFSI**

Ndoo, vyombo vya chakula (sahani. kikombe, bakuli na kijiko). Toilet paper (5 au Zaidi) (vyoo vya maji) tochi(solar), taulo na malapa ya kuogea.

**Kumbuka pia kuleta fedha ya matumizi binafsi.**

7. **VIFAAVYA USAFI WA MAZINGIRA**
    i. Jembe na mpini Wake-1
    ii. Squeezer- 1
    iii. Ndoo ya kudekia na dekio lake (Mopar with its bucket) -1
    iv. Ufagio wa chelewa - 1
    v. Hard broom (ufagio mgumu)/soft broom (ufagio laini)-1
    vi. Fyekeo au kwanja-1

8. **TAREHE YA KURIPOTI CHUONI**

Chuo kitafunguliwa tarehe 18/08/2025. Ripoti chuoni siku na saa za kazi (saa 1.30 asubuhi hadi 09.30 jioni). Tarehe ya Mwisho ya kuripoti chuoni ni wiki mbili tu tangu tarehe ya kufungua chuo.

**ANGALIZO: Atakayefika chuoni baada ya tarehe ya Mwisho ya kuripoti hatapokelewa.**

9. **Mawasiliano:**

Mkuu wa Chuo -0763559333, Makamu wa Mkuu wa Chuo-0762711196, Mwadili 0764954779, Msajili-0769826967, Mratibu Taaluma – 0763391930.
**MUDA WA MAWASILIANO NI: Siku za kazi kuanzia siku ya Jumatatu – Ijumaa Muda ni 07:30Asubuhi mpaka 15:30 Alasiri.**

10. **KANUNI NA SHERIA ZA CHUO**

Soma kanuni na Sheria za Chuo zilizoambatanishwa na uzielewe mapema. Ukifika chuoni utapewa maelekezo zaidi pamoja na kujaza fomu ya kukubaliana na sheria na taratibu za

## KANUNİ NA SHERIA

### UTANGULIZI

"Ubora mkubwa zaidi wa kazi ya Mwalimu upo katika kufundisha watu kwa mifano yake ya matendo mema. "Maisha ya Mwalimu” (S. K Mgoma, H.T.Chowo, S.K Lipiki).

İli kumpa Mwanachuo madaraka kamili juu ya tabia yake, Chuo kina kanuni na sheria zifuatazo ambazo ni mwongozo wa nidhamu na malezi bora.

A. **Sheria za Nchi**

Kila mwananchuo anatakiwa afuate sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kuwa mwanachuo Siyo kinga ya kutofuata sheria za Jamhuri.

B. **Mafunzo**

Shughuli zote zilizopangwa katika ratiba ni muhimu. Kila mwanachuo anawajibika kuhudhuria vipindi vvote na kutekeleza shughuli zilizopangwa kwa bidii.

C. **Maadili**

i. Kuwa na kiasi katika mambo ya starehe.

ii. Ni kosa kuwa katika hali ya kulewa (ulevi wa aina yoyote).

iii. Zingatia kuwa, mazoea ya kuvuta sigara Siyo mazuri kwa afva, usivute sigara katika maeneo yafuatayo: - Maktaba

- Darasani
- Bwalo la chakula
- Katika mikutano
- Mbele ya wakuu wako

iv. Zingatia kanuni za usafi kwa kujiweka wewe mwenyew na mazingira ya chuo chako katika hali ya

v. Vaa mavazi ya heshima uwe na haiba nzuri ya kiualimu.

vi. Waheshimu walezi wako, walimu,viongozi, wageni na wanachuo wenzako hapa chuoni na nje ya chuo. Siku zote kuwa kielezo chema cha mtu aliyeelimika, ambaye kwake Elimu ni Ukombozi.

vii. Wanachuo yawapasa kuishi kama ndugu au kwa uhusiano wa kaka na dada, hivyo ni kosa kwa wanachuo kuwa na mahusiano ya kimapenzi

Viii. Tunza majengo na Vifaa vyote vizuri ili vikufae wewe leo na vizazi vijavyo.

ix. Uwe mwaminifu mwenye haki na mkweli kwa kila usemalo na ütendalo.

x. Chakula kitaliwa katika bwalo la chakula, hairuhusiwi kupeleka au kula chakula bwenini.

xi. Huruhusiwa kuwa na Vifaa vya ina yoyote ile vinaweza kuleta hatari ya moto bwenini. Vifaa hivyo ni pamoja na jiko la mafuta ya taa, au umeme, hita (heater), sufuria,pressure cooker na "music systeam”

xii. Wahi wakati wote mahali unapohitajika yaani darasani,bwaloni,ukumbini,katika kazi ya njee, unapoitwa kwa kengele au ishara nyingine.

xiii. Huruhusiwi kutumia simu yako wakati wa kipindi au katika makusanyiko rasmi ila kwa ruhusa maalum (utapaswa kuzima simu yako)

D. **Matembezi**

i. Matembezi nje ya mji wa Monduli lazima upate kibali maalum kutoka kwa Mwadili.
ii. Ruhusa zote za kulala nje ya chuo au kuwa nje ya chuo usiku ni lazima upate kibali cha Mkuu wa Chuo iii. Ruhusa ndogo za kutoka nje ya chuo wakati wa shughuli rasmi, zitatolewa na Mkufunzi wa zamu au Mwadili.
iii. Hairuhusiwi kutembelea nyumba za watumishi wa chuo bila idhini maalum kutoka kwa Mwadili au Mkufunzi wa zamu.
iv. Wanachuo wa kike au wa kiume ni marufuku kuingia katika mabweni yasiyo yajinsi yake.
v. Wanachuo wakiwa nje ya chuo, ni marufuku kuingia sehemu za kuuzia vilevi/pombe, nyumba za wageni, au sehemu nyingine zinazofanana na hizo.
vi. kuhakikisha upo ehuoni wakati wote, zitakuwepo "Roll Call" kwa muda utakaopangwa kubwa kutokuhudhuria "Roll Call" na makusanyiko mingine iliyo rasmi vii. Wageni wa wanachuo wataruhusiwa wakati wa mapumziko hasa siku za Jumapili na Jumamosi mchana. Wageni hawaruhusiwi kuingia madarasani, mabwenini au bwaloni.

E. **Mikutano na Mawasiliano**

i. Mikutano na mikusanyiko ya aina yoyote ya wanachuo hapa chuoni ni lazima ijulikane rasmi, kwa kupatiwa kibali kutoka kwa Mwadili na Mkufunzi wa zamu kabla ya kukutana.
ii. Taarifa itolewe mapema kwa Mkuu wa Chuo, kuhusu mikutano na michezo baina ya wanachuo na jumuiya za nje ya chuo ili kupata kibali kabla ya kukutana.
iii. Mazungumzo ya faragha kati ya wanachuo yafanyike mahali pa wazi na siyo kwenye maficho au mahali pa giza.
iv. Barua zote za shughuli rasmi/kiofisi zipitie kwa Mkuu wa Chuo. Pia taarifa zote zinazotakiwa zishughulikiwe kiofisi, ziandikwe kwa Mkuu wa Chuo.

## TAHADHARI KWA WANACHUO

Yafuatayo ni mambo ambayo yanaweza kumfanya mwanachuo aondolewe katika mafunzo bila maonyo ya awali. Jihadhari nayo.

i. Wizi
ii. Matumizi ya Simu bila Ruhusa
iii. Utoro

iv. Uzinzi
v. Kuwa mjamzito
vi. Kutoa mimba
vii. Kupiga/kupigana na mtu yeyote
viii. Kugoma
ix. Ulevi
x. Uhuni kwa mbinu mbalimbali
xi. Kosa la jinai kuvunja sheria za nchi
xii. Kushawishi wanachuo/watu wengine wavunje sheria za nchi/chuo
xiii. Kuharibu mali/Vifaa kwa makusudi (malicious damage to property)

Prof.Samwel M. Irira

PRINCIPAL
MONDULI TEACHERS COLLEGE
P. O. Box 5 MONDULI

**MKUU WA CHUO**

GOVERNMENT OF TANZANIA REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PRINCIPAL
MONDULI TEACHERS COLLEGE
P. O. Box 5 MONDULI

FROM: THE PRINCIPAL,
MONDULI TEACHERS' COLLEGE.

P.O. BOX 5, MONDULI.

DATE: ...................

PART A
TO: The Medical officer

__________________________

__________________________

...............................................

S/N:

REF: - MR/MRS/MISS. ................................

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full-time teacher training course. The examination should include all categories (I-V). Each category or sub-category will render the applicant ineligible in case of defect. I.

(a) Eye Sight (e) Peptic Ulcers (i) Urine analysis
(b) Leprosy (f) Stool analysis (j) Limbs
(c) WBC (g) Speech (k) Tuberculosis
(d) Hearing (h)Epilepsy (l) Venereal Diseases

Il. Neuroses
Ill. Other Serious Diseases
IV. Pregnancy
V. Mental and physical Fitness

PART B**: MEDICAL CERTIFICATE**

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for a full-time teacher training course.

I. (a) Eye Sight. . . ....(t) Leprosy
. . . .. ...(g) Epilepsy...........
(b) Hearing ... (e) Speech. ..
Ulcers.. .......(h) Peptic

(d) Venereal Diseases. (i) Tuberculosis.. (e)
Limbs.....................................

11. NEUROSES....

.........................................................................................

111.Other serious Diseases.

.........................................................................

IV. Pregnancy.... ________________ ..........................................................

V. Mental and Physical Fitness.................................................................................

Date .................................. Signature.....................................................

Station... ............................ Designation. .. . . ............